MATUMAINI PROG NO:2428

TITLE: THE LAST COVENANT (Part Three)

SUMMERY: KINAANGAZIA KUHUSU KUKAMILIKA KWA AGANO.

TEXT: YEREMIA 31:31-34

MADA: AGANO LA MWISHO (Sehemu ya tatu)

……

Ni wakati mwingine wa kuhesabu baraka maana Mungu wetu ametuweka hai tena ili tukaweze kujifunza kutoka kwenye Neno lake takatifu ambalo ni Bibilia.

Naichukua tena nafasi hii ili kukusalimu na Zaidi sana kukukaribisha kwa upendo wake Mwenyezi Mungu popote ulipo mpendwa.

Ningependa kwanza kabisa tuombe Kabla ya kuendelea na somo la leo.

Na tuombe;

OMBI….Mungu mkuu na tena Baba Yetu uliye mbinguni, ni wakati mwingine tunapokushukuru kwa nafasi hii ambayo umetupatia ili kujifunza hili neno lako kuhusiana na Agano hili la mwisho sehemu ya tatu.

Tunaomba roho Wako Akatuongoze katika kulielewa .Ni kwa Yesu tumeomba …..Amen

Ninalotumaini ya kwamba Mwenyezi Mungu Angali amekuweka hai kupitia kwa upendo Wake ambao ni Mkuu.

Hiki nikipindi cha Matumaini kutoka TWR Nairobi.

Kwenye somo hili la leo,,tunajifunza kulihusu Agano la Mwisho hii ikiwa ni (Sehemu ya tatu)

Somo hili bado tunalitoa kwenye Yeremia 31:31-34.

Kwa kumalizia kipindi hiki cha leo mpendwa,,nitakuwa nakupatia anwani yangu kwa sababu ya mawasiliano kati yangu nawe.

Jina langu ni Vincent Amara.

Kwa upole nakuomba uniruhusu kwanza kukubariki na wimbo huu,Damu Ya Yesu Husafisha kabisa

WIMBO: .....

Shukran sana waimbaji wetu kwa wimbo huu mzuri hivyo,, yaani damu ya Yesu husafisa kabisa.....

Karibu tena kwenye kipindi hiki cha Matumaini kutoka TWR ambapo leo hii ,,,,tunajifunza kulihusu Agano la mwisho(Sehemu ya tatu) huku somo bado likitoka kwenye kitabu cha Yeremia 31:31-34. Nitaunganisha pia na vifungu kutoka kwenye vitabu vingine.

Mpendwa kama ambavyo tumejifunza kuhusiana na maagano,,tunaweza kuona

wazi kabisa ya kwamba,,lengo la maagano hayo ni kwamba mwanadamu aweze

kumfahamu Mwenyezi Mungu jinsi alivyo.

Tukiyatathimini maagano hayo,,tunaona jinsi ambavyo Mwenyezi aliyatayarisha na pia kuendelea kuyafanya kuwa hata magumu Zaidi. Sababu Yake ilikuwa ni watu wote wapate kukamilishwa katika Agano la Ukamilifu.

Msikilizaji wangu,,kwa kulichambua neno Zaidi,,tunaona ya kwamba,,,Agano la Mwisho litatimia tu,,wakati ambapo,,,kila mtu atamjua Bwana.

Kwa wakati huu,,,tunangoja tu,,,kutimia kwa Unabii ulionenwa na Yeremia katika 31:31-34, ili Agano likamike.

Unabii huo unasomeka hivi;

31. Tazama, siku zinakuja, asema Bwana, nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda;

32. Si sawasawa na agano lile nililofanya na baba zao, siku ile nilipowashika mkono ili kuwatoa katika nchi ya Misri; ambalo agano langu walilivunja, ingawa nalikuwa mume kwao, asema BWANA;

33. Lakini agano hili ndilo nitakalofanya na nyumba ya Israeli; Baada ya siku zile, asema Bwana, nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu.

34 Wala hawatamfundisha kila mtu jirani yake, na kila mtu ndugu yake, wakisema, Mjue Bwana;

Agano hili liloandikwa na Nabii Yeremia ndilo la mwisho na wala hamna jingine,,,Rafiki yangu.

Ni jambo la muhimu kuelewa kuhusu ukweli huu. Mariamu mama wa Yesu alipochukua mimba kwa nguvu za Roho Mtakatifu,,,Malaika Gabrieli Alimwiita Kristo,,,Mwana wa Aliye Juu. Hayo yameandikwa kwenye Injili ya Lika Mtakatifu 1:30-33

Mungu wetu Alijivika mwili wa mwanadamu na kuteremka humu duniani kupitia kwa bikira,,ili kuukomboa ulimwengu kwa sababu Adamu na Hawa walifanya dhambi katika bustani ya Edeni.

Kila mtu aliyezaliwa na Adamu na Hawa bila shaka ni mwenye dhambi.

Kwa muujiza wa kuzaliwa kwa Yesu na bikira, alikuwa mwanadamu kweli, lakini hakuwa na asili ya dhambi maana,, Bibilia inatufundisha ya kwamba hakutenda dhambi kamwe.

Kitabu cha Waebrania 4:15,,neno linasema “Kwa maana hatuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu, bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote bila kufanya dhambi,”.

Kwa hivyo, katika mpango wa Mungu wa kumfanya Kristo kuwa Mtakatufu,,Yeye alifanyika dhabihu ya kutupatanisha naye.

Mtume Paulo akiwaandikia Wakorintho katika barua yake ya pili 5:21 alisema, “Kwa maana yeye (akimaanisha Mungu) alimfanya (akimaanisha Yesu) yeye asiyejua dhambi kuwa dhabihu ya dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu ndani yake,”.

Kwa hivyo, kwa Imani,,,Kristo Alikufa nasi.

Tunapoendelea na kuichambua Bibilia,,,tunaona ya kwamba Mtume Paulo katika 2 Wakorintho 5:14, 15 alieleza hilo vilevile . Alisema“Kwa maana upendo wa Kristo watubidisha, kwa kuwa tunahukumu hivi kwamba mtu mmoja alikufa kwa ajili ya wote, basi wote wamekufa;

Kutoka katika Mwanzo 22:13,, tunamwona Abrahamu akimbadilisha mwanawe Isaka na kondoo wa kiume juu ya madhabahu ambapo kondoo huyo aliuwawa badala ya Isaka. Kwa hivyo fundisho la kuingizwa limejikita katika Agano la Kale katika uzoefu wa Ibrahimu.

Naye Nabii Isaya akiandika katika Sura yake ya 53:4-6 kumhusu Kristo,,, alisema hivi “Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu.Alichubuliwa kwa makosa yetu ,Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo

tumepotea,Kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe,Na Bwana ameweka juu yake Maovu yetu sisi sote

Rafiki yangu,,hakuna neno lililo wazi zaidi linaloweza kutolewa kuhusu ubadilishanaji huu. Mungu Alishuka kama mwanadamu humu ulimwenguni kwa njia ya Kristo na Akatubebea dhambi zetu pale Msalabani Kalvari. Bila shaka kwa wote wamwaaminio waurithi ufalme wa Mbinguni Pamoja naye.

Yesu alikutana na wanafunzi wake usiku wa kusulubiwa kwake ili kula Pasaka pamoja nao. Walipokuwa wakila, Yesu akakitwaa kikombe. Akashukuru, akawapa wanafunzi wake kikombe, akasema, Nyweni nyote katika kikombe hicho.

Kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano jipya, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi," Mathayo 26:27, 28.

Injili za Marko na Luka zinatupa masimulizi sawa ya tendo hili la Yesu ili kuonyesha kwamba damu yake iliyomwagika ndiyo msingi wa msamaha wetu.Kristo Aliiita agano jipya ambalo ndilo Agano la Mwisho.

Maagano mengine yalitegemea mwitikio wa utii wa wale ambao agano lilifanyika nao. Kuvunjika kwa Agano pia,,kulitegemea kutotii kwa wale ambao walipewa Agano. Kumbuka tu ya kwamba,,,katika kila Agano,,Mungu Aliweka masharti.

Tukisoma neno kwenye Waebrania 4:15 na 2 Wakorintho 5:21,,tunaona ya kwamba,,Agano Jipya halikuvyunjwa maana Kristo aliishi Maisha Matakatifu.

Pamoja na hayo, kwa sababu Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, Yeye ndiye anatupatanisha na Mungu. Mwandishi wa Waebrania katika sura yake ya 7:14-17 anatuonyesha uhusiano wa ukuhani wa Melkizedeki na ukuhani wa Yesu.

Hii ina maana ya kwamba hakutakuwa na ukuhani mwingine baada ya ukuhani wa Yesu

……

"Na ni dhahiri ya kwamba Bwana wetu alitoka katika Yuda, kabila ambayo Musa hakunena neno lo lote katika habari ya ukuhani. Na bado ni dhahiri zaidi ya kuwa ametokea kuhani kwa mfano wa Melkifsedeki, ambaye amefanywa, si kwa sheria ya amri iletayo amri ya mwili, bali kuhani asiye na uzima, bali kuhani asiye na uzima. milele baada ya utaratibu wa Melkizedeki."

Anaendelea tena katika sura yake ya 7:26-28,,na kusema "Kwa maana ilitupasa sisi kuhani mkuu wa namna hii, aliye mtakatifu, asiye na hatia, asiye na uchafu, aliyetengwa na wakosaji, aliye juu kuliko mbingu; asiyehitaji kila siku, kama wale makuhani wakuu, kutoa dhabihu kwanza kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe, kisha kwa ajili ya dhambi za watu; udhaifu; bali neno la kiapo lililokuwako baada ya torati, limemteua Mwana, aliyetakaswa hata milele,"

…….

Hatimaye katika Waebrania 9:11-12 tunafundishwa kwamba hakuna dhabihu nyingine ya kutosha dhambi zetu ila Damu yake Yesu.

Ndugu yangu,,Dhabihu ya Yesu ndiyo pekee ya kutuondolea dhambi, na hakuna kurudiwa tena. Neno linasema "Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu; vivyo hivyo Kristo naye alitolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi;

Kama ambavyo tumekuwa tukijifunza neno,,tunaona ya kwamba Maagano mengine yote yametuelekeza kwenye Agano jipya yaani, Agano la Ukamilifu.

Agano hili lilihahidiwa na Yeremia,, na,,, kuzinduliwa na Yesu katika kifo chake msalabani. Kutekelezwa kwake kamili kunangoja kuthibitishwa na wale ambao Mungu alisema ataifanya nao, yaani nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda.

Siku hiyo mpendwa inakuja na Zaidi sana inakaribia.

Ni Mungu tu ndiye anaiyejua maana hata Kristo Mwenyewe Alisema haijui.

Yeye binafsi atasimamia mambo, akithibitisha Jina Lake Takatifu na kutimiza kila ahadi Aliyotoa!

Agano la Yeremia litakapothibitishwa na nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda, litakuwa ni Agano la Ukamilifu. Ndani yake maagano yote yaliyotangulia yatakamiliswa kama vile ilivyokusudiwa na Mungu Mwenyewe.

Dadangu,,Mungu atalikamilisha Agano la Utawala wakati Mwanadamu Mkamilifu atakapokuwa na mamlaka kamili kama vile Mungu alimpa Adamu mara ya kwanza wakati wa uumbaji.

Mungu atakamilisha Agano la Ukombozi katika ushindi wa mwisho wa Uzao wa mwanamke juu ya uzao wa nyoka katika kuponda kichwa cha nyoka na kumpeleka kwenye moto wa milele.

Mwenyezi Mungu atalikamilisha Agano la Kuhifadhi atakapowakusanya Waumini kwake mbinguni huku akiitakasa ardhi katika hukumu ya mwisho.

Mungu atakamilisha Agano la Uchaguzi wakati uzao wa Ibrahimu, Israeli, utakapokuwa kile neno linasema"kichwa na wala si mkia."

Mungu atakamilisha Agano la Utakaso huko Yerusalemu kwa ajili ya wateule wake.Kwa neema na rehema atasamehe maovu yao yote.

Mungu atalikamilisha Agano la Makao kwa kuyakusanya tena pamoja makabila yote kumi na mawili katika nchi yao ya ahadi.

Rafiki yangu,,,Mungu atakamilisha Agano la Utawala wakati Mwana wa Daudi, Yesu, Masihi, atayatawala mataifa kwa fimbo yake ya chuma; Utawala wake utaenea kutoka bahari hadi bahari. Neno linasema ya kwamba,,,Mataifa yote yatamsujudia.

Agano la mwisho lililotangazwa na Yeremia litakuwa kilele na onyesho la utoaji wa neema ya Mungu kwa wanadamu wote. Mtiririko wa historia unatuelekeza kwenye siku hiyo kuu ya hukumu,,Naye Mhukumu wa haki ambaye ni Mwenyezi Mungu.

Kwa hivyo msikilizaji wangu,,,jibu la swali letu, kwamba,,,ni,, Nani Anayesimamia Historia?, lazima limfedheheshe mwanasiasa mwenye kiburi ambaye mwisho wake uko mkononi mwa Mwenyezi Mungu; lazima iwategemeze wanyenyekevu na waliotubu,,, wanaoelewa na kudai neema ya Mungu,,,kama inavyomiminwa kwa upendo juu ya wenye kutubu.

OMBI. Baba yetu wa Mbinguni na Zaidi sana Mfalme Uliyetukuka zaidi ya vyote. Kupitia kwa somo la leo,tunasema ni asante kwa ajili ya ufunuo huu kulihusu Agano hili la mwisho.

Tunakuomba ukatuwezeshe katika kulitilia maanani kupitia kwa usaidizi wa Roho Wako.

Ni kupitia kwa Jina la Bwana wetu Yesu Kristo…..Amen.....

Mpendwa,,Kimekuwa ni kipindi chako cha kujifunza neno Lake Mwenyezi Mungu.Kipindi cha matumaini kutoka Twr.Leo tumejifunza kulihusu Agano la mwisho(Sehemu ya Tatu) huku somo likitoka kwenye kitabu cha Yeremia 31:31-34.

Nitakuomba uwasiliane nami kupitia kwa anwani nitakayo shiriki nawe mwishoni mwa kipindiki hiki cha leo. Anwani hiyo ni kwa ajili ya kusaidiana nawe.

Kabla yake,,,ni wimbo…damu ya Yesu inanena mema_Herbert_ft_Esau Tosh_&_Henry the band

WIMBO…….

Ni wimbo damu ya Yesu inanena mema_Herbert_ft_Esau Tosh_&_Henry the band

ANDIKA BARUA AU UJUMBE WAKO UKIANZA NA NENO MATUMAINI TWR NA KUTUMA KWA:

SLP 21514 CODE 00505

NAIROBI KENYA x2
Simu/Sms 0721970520 x2
Barua Pepe-barua@twr.co.ke

Mpendwa,,nakuombea baraka zake Mwenyezi Mungu,,popote ulipo na,, hadi wakati mwingine, jina langu ni Vincent Amara……Kwaheri